

Muhtasari wa Ukurasa Mmoja wa Uthibitisho wa Majoribio ya Matibabu ya Ivermectin kwa COVID-19

Ivermectin, dawa ya kupambana na vimelea ambayo ugunduzi wake ulishinda Tuzo la Nobel katika mwaka wa 2015, imethibitika kuwa yenye nguvu sana, inapambana na virusi na vilevile uvimbe kulingana na utafiti wa maabara. Katika miezi 4 iliyopita, majoribio mengi ya kimatibabu yaliyodhibitiwa kutoka katikavitu na nchi nyingi ulimwenguni pote yanaripoti ongezeko kubwa la ubora na uthabitii katika matokeo ya wagonjwa wa COVID-19 wanapotibiwa kwa kutumia ivermectin. Ukaguzi wetu kamili wa kisayansi wa majoribio haya yaliyorejelewa unaweza kupatikana kwenye seva ya Open Science Foundation kabla ya kuchapishwa hapa: <https://osf.io/wx3zn/>.

Sifa za Ivermectin

- 1) Ivermectin huzuia kuzaana kwa virusi vingi, kutia ndani SARS-CoV-2, mafua, na vingine;
- 2) Ivermectin ina nguvu ya kupambana na uvimbe na mbinu nyingi za kuuzuia;
- 3) Ivermectin hupunguza ukali wa virusi na hulinda dhidi ya uharibifu wa viungo katika wanyama;
- 4) Ivermectin huzuia maambukizi ya COVID-19 inapotumiwa kabla au baada ya mfiduo;
- 5) Ivermectin huharakisha kupona na hupunguza muda wa kulazwa hospitalini na vifo ya wagonjwa walio na COVID-19;
- 6) Ivermectin hupunguza idadi yavifo katika maeneoambayo matumizi yake yameenea.

Uthibitisho Msingi Unaounga Mkono Ufanisi wa Ivermectin katika COVID-19 kufikia Januari 11, 2021

(RCT = majoribio yaliyodhibitiwa bila mpangilio hususa, OCT = majoribio ya kutazama yaliyodhibitiwa). Kila jaribio la kitiba linaonyesha manufaa, huku RCT na OCT ziikipoti mwelekeo sawa na ukubwa; karibu zote ni muhimu kitakwimu.

Majoribio yaliyodhibitiwa kutafiti uzuiaji wa COVID-19 (majoribio 8 yamekamilika)

- RCT 3 zilizo na upungufu mkubwa wa kitakwimu katika viwango ya maambukizi, jumla ya wagonjwa 774
- OCT 5 zilizo na upungufu mkubwa wa kitakwimu katika viwango ya maambukizi, jumla ya wagonjwa 2,052

Majoribio yaliyodhibitiwa katika matibabu ya wagonjwa wa mapema na waliolazwa hospitalini wa COVID-19 (majoribio 19 yaliyokamilika)

- RCT 5 zilizo na upungufu mkubwa na muhimu katika muda wa kupona au urefu wa muda wa kulazwa hospitalini, jumla ya wagonjwa 774
- RCT 1 iliyo na upungufu mkubwa wa kitakwimu katika kiwango cha kuzorota/kulazwa hospitalini, jumla ya wagonjwa 363
- RCT 2 zilizo na upungufu mkubwa katika ukali wa virusi, siku za kupotea kwa uwezo wa kunusa, kukohoa, au muda wa kupona, jumla ya wagonjwa 85
- RCT 3 zilizo na upungufu mkubwa wa vifo, jumla ya wagonjwa 695
- OCT 3 zilizo na upungufu mkubwa kitakwimu wa vifo, jumla ya wagonjwa 1,688

Idadi ya Tafiti na Wagonjwa Miiongoni mwa Majoribio ya Kitiba yaliyopo ya Ivermectin katika COVID-19

- Majoribio 27 yaliyodhibitiwa, kutia ndani jumla ya wagonjwa 6,612 yamekamilishwa kwa kutumia vikundi vinavyofaanu vilivyoedhibitiwa
- Majoribio 16, kutia ndani zaidi ya wagonjwa 2,500 ni tafiti zinazotazamiwa, zisizo na mpangilio hususa, na zilizodhibitiwa
- 11 kati ya majoribio 27 yamechapishwa katika majorida yaliyopitiwa na marika, wagonjwa 3,900, yanayosalia yanayosubiri kuchapishwa

Ushirikiano wa Mstari wa Mbele wa Huduma Muhimu wa COVID-19 – Mapendezo ya Ivermectin katika COVID-19

Hata mipaka inapowekwa na kuzingatia tu uchambuzi wa majoribio 16 yaliyodhibitiwa (jumla ya wagonjwa 2,500), idadi kubwa zaidi huripoti upungufu mkubwa wa maambukizi kitakwimu au kuongezeka kwa ugonjwa au idadi ya vifo. Zaidi ya hayo, uchambuzi-mpevu uliofanywa hivi karibuni na muungano huru wa utafiti ulihesabu uwezekano wa ivermectin kuwa hafifu dhidi ya COVID-19 kuwa 1 kwa milioni 67.¹

FLCCC Alliance, kulingana na uthibitisho wa jumla uliopo, inaunga mkono pendekezo la A-I (utaratibu wa viwango wa NIH; kiwango cha nguvu, uthibitisho wa hali ya juu) kwa matumizi ya ivermectin katika uzuiaji na matibabu ya awamu zote za COVID-19.

Zaidi ya hayo, tunahimiza mashirika yote ya udhibiti yakague hati yetu inayoeleza tafiti zilizotajwa awali na vilevile “majoribio asili” ya idadi kubwa ya watu yaliyotokea katika miji na mikoa mingi baada ya kuanza kwa mipango ya usambazaji wa ivermectin.² Matumizi yaliyoenea ya ivermectin yaliyotokeza upungufu mkubwa wa visa na idadi ya vifo ambavyo vilikaribia viwango vya kabla ya janga katika maeneo haya. Kama inavyothibitishwa na yale yaliyotokea katika maeneo haya, ivermectin inaonekana wazi kuwa sehemu muhimu na ya lazima katika kufikia udhibiti wa janga hili.

¹ ivmmeta.com

² Kory P, Meduri GU, Iglesias J, Varon J et al. Ukaguzi wa Uthibitisho Unaojitokeza Kuonyesha Ufanisi wa Ivermectin katika Uzuiaji na Matibabu ya COVID-19. Open Science Foundation. <https://osf.io/wx3zn/>